**MUONGOZO WA KUJISAJILI KUSAMBAZA NA KUTOA BIDHAA NA HUDUMA MTAMBUKA KUPITIA MFUMO WA USIMAMIZI WA UNUNUZI WA UMMA KIELEKTRONI - NeST**

Bidhaa au huduma mtambuka (Commonly Used Items and Services) ni bidhaa au huduma muhimu zinazonunuliwa mara kwa mara na taasisi nunuzi.
Taasisi nunuzi zinapaswa kununua bidhaa au huduma mtambuka kwa wazabuni walioingia kwenye makubaliano ya kimkataba (Framework Agreement).

Makubaliano haya ya kimkataba yanaruhusu taasisi nunuzi kununua bidhaa au huduma zinazohitajika kwa mwendelezo au zinazojirudia, kupitia kutoa oda kadhaa.

Ili kuongeza ufanisi na kupunguza muda wa ununuzi wa huduma na bidhaa mtambuka zinazotumiwa na taasisi nunuzi zote, mfumo wa NeST unawaruhusu wazabuni waliosajiliwa kwenye aina za biashara zinazohusika na usambazaji wa bidhaa na utoaji wa huduma mtambuka, kusaini makubaliano ya kimkataba (Framework Agreements) zitakazowawezesha kusambaza bidhaa na huduma hizo kwenye taasisi nunuzi.

**A. Kujua aina za biashara (business lines) za bidhaa au huduma mtambuka**

Ili kujua aina za biashara zinazohusika na usambazaji wa bidhaa au utoaji wa huduma mtambuka, ingia kwenye mfumo kwa kutumia taarifa zako za utambulisho.
Bofya **Frameworks**, kisha bofya **Business Lines**.




## B. Kujisajili kusambaza bidhaa au kutoa huduma mtambuka

Ili kuchagua aina za biashara unazoweza kuingia na kusaini makubaliano ya kimkataba ya huduma na bidhaa mtambuka;

a. Bofya **Frameworks**, kisha…;

b. Bofya **Framework**;

PPRA

Public Procurement Regulatory Authority




c. Bofya **Create;**

d. Sehemu ya ***Select business line*****,** chagua aina ya biashara ulizojisajili kufanya ambazo unaweza kuingia makubaliano ya kimkataba ya bidhaa na huduma mtambuka;




e. Bofya **Continue** kuendelea, kisha **Yes** kukubali;

f. Kwa kila biashara uliyochagua kuingia makubaliano ya kimkataba ya bidhaa na huduma mtambuka, utaweza kuona na kupitia orodha ya bidhaa au huduma ulizojiandikisha kusambaza au kutoa;




g. Bofya **Submit** kuwasilisha, kisha **Yes** kukubali;

## C. Kusaini makubaliano ya kimkataba ya bidhaa na huduma mtambuka (framework agreement)

Itafunguka nyaraka ya makubaliano ya framework, yenye vigezo na masharti ya kusambaza bidhaa na kutoa huduma mtambuka.

Public Procurement Regulatory Authority




h. Soma kwa umakini vigezo na masharti, kisha saini kwa kuingiza ***neno siri*** lako (Keyphrase);




i. Bofya **Sign and Continue** kuendelea;

j. Unaweza kuona nyaraka ya makubaliano uliyosaini kwa kubofya ikoni ya jicho. Nyaraka ya makubaliano uliyoyasaini itafunguka. Unaweza

kuipakua kwa kubofya ikoni ya kupakua au kuuchapa kwa kubofya ikoni ya kichapishi;

k. Ili kuhuisha au kufanya marekebisho ya makubaliano, bofya ikoni ya kuhariri;




l. Unaweza pia kufuta au kujiondoa kwenye makubaliano kwa kubofya ikoni ya kipipa;

**Muhimu:** Ukifuta au kujiondoa kwenye makubaliano ya kusambaza bidhaa au kutoa huduma mtambuka, hautaweza kupata tena mialiko ya zabuni za bidhaa au huduma mtambuka. Hivyo, utatakiwa kukamilisha zabuni zote ambazo umekubali na kujifunga kufanya.

## D. Historia ya makubaliano ya Framework

Sehemu ya **Framework History,** utaweza kuona kumbukumbu ya makubaliano yote ya kusambaza na kutoa bidhaa na huduma mtambuka uliyoingia.




Hadi kufikia hapo, utakuwa umeingia kwenye makubaliano ya kusambaza na kutoa bidhaa na huduma mtambuka. Taasisi nunuzi zitakapotangaza zabuni za bidhaa au huduma mtambuka, mzabuni aliyesaini makubaliano ya hayo atapata mwaliko wa zabuni kwenye anuani ya paruapepe yake.